

HALMASHAURI YA WILAYA YA MPIMBWE

Unapojibutafadhali taja:

Barua pepe: ded@mpimbwe.dc.go.tz
Tovuti: www.mpandadc.go.tz



S.L.P 245,

MPANDA-KATAVI.

Kumb. Na. KTV/MPDC/H.10/1 VOL II/71

17 Septemba, 2019

YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mpimbwe kwa kushirikiana na Shirika la **Walter reed** anapenda kuwatangazia wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi moja (1) ya Ajira ya Mkataba wa mwaka mmoja (1) kwa nafasi ya **Afisa Takwimu (Data Manager)** na nafasi nane (8) za **Makarani wa Takwimu (Data clerks)** kama ifuatavyo:-

1.0 Afisa Takwimu (Data Manager)- Nafasi (1)

1.1 Majukumu yake:

- i. Kufanya kazi za uchambuzi wa taarifa na kuandaa taarifa ili kurahisisha tathimini kwa ngazi ya Wilaya;
- ii. Kusimamia uingizaji wa taarifa kwa usahihi kwenye kanzi data ya CTC2 ipasavyo
- iii. Kuhakikisha taarifa za CTC2 zinaingizwa siku hiyo hiyo baada ya kutoka kwa Daktari
- iv. Kuhakikisha kanzi data ya CTC2 inahuishwa kila inapohitajika,
- v. Kuhakikisha Mfumo wa CTC2 unafanya kazi kwa usahihi ikiwa ni pamoja na ubora wa takwimu
- vi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi au Msimamizi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali katika Utumishi wa Umma.

1.2 Sifa za Mwombaji;

- i. Kuajiliwa mwenye Shahada ya Takwimu au Hisabati au sifa zinazolingana na hizo kutoka Chuo Kikuu kinachotambuliwa na Serikali na mwenye ujuzi wakutumia Kompyuta,
- ii. Awe na Uzoefu wamasuala ya takwimu za Afya (Health Data experience)
- iii. Awe na uzoefu wakutumia mfumo wa DHIS2, Ms Excel, Ms Access, SPSS na uzoefu wa Mifumo mingine itakuwa ni sifa ya nyongeza

1.3 Ngazi ya mshahara

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali yaani TGS D1.

1.4 Makarani wa Takwimu (Data Clerks) Nafasi (8)

1.5 Majukumu yake;

- i. Kufanya kazi za uchambuzi wa taarifa na kuandaa taarifa ili kurahisisha tathimini;
- ii. Kuingiza taarifa kwenye kanzi data ya CTC2
- iii. Kupanga mafaili ya Wagonjwa ili kurahisisha upatikanaji
- iv. Kuhakikisha faili zinaingizwa siku moja tu baada ya kupokea faili toka kwa Daktari
- v. Awe na uzoefu wa masuala ya takwimu za Afya (Health Data experience)
- vi. Awe na uzoefu wakutumia mfumo wa DHIS2, Ms Excel, Ms Access, SPSS na uzoefu wa Mifumo mingine itakuwa ni sifa ya nyongeza;
- vii. Kuhuisha (Update) CTC2 kila inapohitajika
- viii. Kufanya kazi kwenye Vituo vya jirani kusaidia kuingiza takwimu mbalimbali
- ix. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wakazi,

1.6 Sifa za Mwombaji:

Kuajiliwa mwenye Cheti (Certificate) ya Takwimu kutoka Chuo cha Takwimu cha Afrika Mashariki (The Eastern Africa Statistical Training Centre) au Vyuo vingine vinavyotambuliwa na Serikali na wenye ujuzi wa kutumia Kompyuta

1.7 Ngazi ya Mshahara

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali yaani TGS B1 kwa Mwezi.

1.8 MASHARITI YA JUMLA KWA WAOMBAJI:


1. Mwombaji Awe Raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45
2. Mwombaji aambatanishe nakala ya Cheti cha Kidato cha Nne, Sita na Ujuzi kulingana na nafasi anayoomba
3. Mwombaji aambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa
4. Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi (CV) akionesha namba za simu na anuani ya kwake pamoja na anuani za wadhamini,
5. Mwombaji aambatanishe picha ndogo (passport size) mbili (2) kwenye barua ya maombi
6. Waombaji waliostafishwa katika utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kwa kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi
7. Mwombaji aandike nyuma ya bahasha nafasi anayoomba.
8. Waombaji watakaokidhi vigezo wataitwa kwenye usaili.
9. Mwisho wa kutuma Maombi ni tarehe 23.09.2019

NB: Uwasilishaji wa vyeti vya kughushi utapelekea kuchukuliwa hatua za kisheria

Maombi yote yatamwe kwa;

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe,
S.L.P 245,
MPANDA - KATAVI.

Imetolewa na;


Erasto N. Kiwale

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MPIMBWE**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA (W) MPIMBWE**